

ubatizo wa kimadhehebu, watakulaliwa katika ushirika? Ubatizo unaokulaliwa siku hizi ni ubatizo mmoja wa Efeso 4, huo ni ubatizo wa Agizo Kuu.

Ubatizo wa kimadhehebu sio ubatizo wa Agizo Kuu. Kwa hiyo mtu hawezi kupokelewa katika kanisa la Bwana kwa ubatizo wake wakimadhehebu.

**Kuwapokea Watu Katika
Kanisa La Bwana
Kwa Ubatizo
Wao
Wakimadhehebu**

For information contact:

International Bible Teaching Ministries
P.O. Box 49494
Cookeville, TN 38506

(Denominational Baptism- Kiswahili)

Endea Tovuti yetu:

www.IBTMinistries.org

Mtunzi:

Ronald D. Gilbet

Kuna wale wanaosema, ni Mungu peke yake anayejua mambo yote kwa hiyo sisi hatuwezi kujua ikiwa mtu amaokoka au amepotea. Mtu hatakiwi kufahamu kila kitu ndipo afahamu kitu chochote. Mtu anaweza kufahamu mapenzi ya Mungu kuhusu swala la wokovu. Mtu anaweza kufahamu kwa kutegemea neno la Mungu, iwapo ametii au hajatii Injili ya Kristo. Yesu alisema katika Yohana 7:17 kwamba, tunaweza kufahamu mafundisho. Katika Yohana 8:32, tunajifunza sio kwamba tunaweza kufahamu ukweli, bali tunapaswa kufahamu ili tuokolewe. Kwa mujibu wa neno la Mungu, tunajifunza kuwa ubatizo wa kimaandiko, huondoa dhambi za mtu na kumweka ndani ya Kristo palipo na baraka zote za rohoni (Mdo.2:47, 22:16, Gal.3:26-27;Efeso 1:13)

Kuwapokea watu wakiwa na ubatizo wao wakimadhehebu, sio kitu kipywa. Jambo hili linazungumziwa, na hata watu wengi wamefanya miaka mia moja zilizopita. Ikiwa mtu anaweza kupokelewa katika kanisa la Bwana kwa ubatizo wake wakimadhehebu, basi ubatizo wa madhehebu ni halali. Ikiwa ubatizo wa kimadhehebu ni halali, basi vitu vifuatavyo vitakuwa kweli:

1. Ikiwa ubatizo wa kimadhehebu ni halali basi, tunaweza kufundishwa uongo, kutii uongo, na bado tukawa tumeokoka. Ili kufanywa huru, mtu anapaswa kufahamu kweli (Yohana 8:32) Umadhehebu hufundisha uongo kuhusu wokovu na kanisa. Mtu atawezaje kusikia uongo, kutii uongo, na kufanyika kanisa la kweli, mwili uliookolewa?

2. Ikiwa ubatizo wa kimadhehebu ni halali basi, kuna njia nyingi za kumwe-ndea Bwana na sio njia moja. Katika Mathayo 7:13-14 Yesu alizungumzia njia mbili: Njia pana na njia nye-mbamba. Yesu hakuamurisha umadhehebu. Kama mtu anaweza kuja kwa Yesu kwa njia alizofanya mwanadamu, Biblia inajipinga. Katika Yohana 14:6 Yesu alisema, "mimi ndiye njia, kweli na uzima: mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi." Katika Efeso 4:4 Paulo alizungumza kuhusu imani moja na mwili mmoja. Je, mwili mmoja unahusisha madhehebu?

3. Ikiwa ubatizo wa kimadhehebu ni halali basi, kuna ingalao waliokoka nje ya kanisa la Bwana. Kuna wezekana na kuwa na Wakristo walioanguka ndani ya mwili wa Kristo, lakini haiwezikani kuwa na waliookoka nje ya mwili au

Kanisa la Kristo(Mdo.2:47) Wokovu ni baraka za kiroho na biblia inasema kuwa , baraka zote rohoni zimo ndani ya Kristo(Efeso 1:13). Njia ile inayomfanya mtu kuwa Mkristo ndiyo njia ile ile inayomfanya mtu kuzidishwa katika kanisa la Bwana(Mdo.2:47)

Katika Mdo.19 tunasoma kuhusu watu kumi na wawili waliokuwa wamebatizwa katika ubatizo wa Yohana. Baada ya kuhubiriwa injili ya Kristo kwa njia iliyo sahihi, walibatizwa kuingia katika Kristo. Wengine siku hizi wangeliwapeka hawa watu 12 katika ushirika lakini sio Paulo. Katika Efeso 4:5 Paulo alitaja Bwana mmoja, imani moja, na ubatizo moja. Ubatizo wa kimadhehebu haujapata baraka za Mungu hata siku moja. (Marko 7:7) Ikiwa Paulo hakuwapokea wale katika Mdo.19, na ubatizo

halali. Kwa mfano wengine wangeliwapeka kwamba, kama mtu alibatizwa akifahamu kwa wakati ule kuwa yalikuwa mapenzi ya Bwana kwake kubatizwa hiyo ingelitosha vizuri sana. Wengine bado wamebisha kwa kusema kuwa, mtu akiamini kuwa ubatizo ni kwa ajili ya dhambi hilo peke yake linatosha na kwa hivyo ubatizo wake ni halali.

Ubishi huu hautafua dafu ukitazamwa kwa mujibu wa maandiko matakatifu ya Mungu. Katika Marko 1:4 tumeongelezwa kuhusu ubatizo wa Yohana, Yohana alitokea akibatiza nyikani, na kuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi." Basi kwa nini tena wale watu kumi na wawili walibatizwa? Walifahamu walipokuwa wakibatizwa kuwa, walikuwa wakifanya mapenzi ya Mungu.. Ubatizo wa Yohana ulikuwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Lakini ubatizo wa Yohana haukuwa ubatizo wa agizo kuu (Mathayo 28:18-20 ; Marko 16:15-16; Luka 24:46-47) Wakati moja ubatizo wa Yohana ulikuwa umekbalika na Mungu ukiwa na mamlaka ya kutoka mbinguni. (Lakini sio tangu Pentekoste baada ya kufufuka kwa Yesu Kristo). Mdo 19:4 inasema kuwa, walifundishwa kuamini Yesu Kristo. Ndugu zetu waliowengi siku hizi, wangeliwapeka hawa watu 12 katika ushirika lakini sio Paulo. Katika Efeso 4:5 Paulo alitaja Bwana mmoja, imani moja, na ubatizo moja. Ubatizo wa kimadhehebu haujapata baraka za Mungu hata siku moja. (Marko 7:7) Ikiwa Paulo hakuwapokea wale katika Mdo.19, na ubatizo